MATUNDASI ASM DEVELOPMENT COMPANY LIMITED

https://www.matundasiasm.co.tz/ info@matundasiasm.co.tz

**28 Mei, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Matundasi ASM Development Company Limited (MADC) ni kampuni inayojishughulisha na utafiti na uchimbaji wa madini katika Mkoa wa Mbeya, wilaya ya Chunya. Kampuni hii inawatangazia wote wenye sifa tajwa kuwasilisha maombi ya kuajiriwa katika nafasi mbalimbali kama ifuatavyo:

**FUNDI MAKENIKA WA MITAMBO MIKUBWA (Heavy Duty Mechanic)**

**FUNDI MAKENIKA WA MITAMBO MIKUBWA DARAJA LA III (Heavy Duty Mechanic III)** Nafasi Moja (01)

**SIFA ZA MUOMBAJI:**

- Awe na cheti cha kuhitimu kidato cha nne (CSEE) au zaidi.
- Awe amehitimu mafunzo ya ufundi stadi wa Daraja la III (Trade Test Grade III) au NVA Level I au II katika fani ya *Heavy Duty Mechanics* au *Mechanical Engineering* kutoka VETA au taasisi nyingine inayotambulika.
- Uzoefu wa angalau mwaka mmoja (01) katika kazi ya matengenezo ya mitambo mikubwa kama vile Bulldozer, Excavator, Tractor, Grader na Malori Makubwa ya Migodini (Mining Dump Trucks).
- Uwezo wa kufanya kazi chini ya usimamizi wa mafundi waandamizi.
- Uwezo wa kutambua matatizo madogo ya mitambo kama vile injini, breki, mfumo wa maji (hydraulics), mfumo wa mafuta, n.k.
- Uwezo wa kufanya ukaguzi wa kawaida (daily inspection) wa mitambo mikubwa.
- Uwezo wa kutumia zana za kawaida za kazi kama vile spana, koleo, jack, na torque wrench.
- Uelewa wa kanuni za usalama kazini (HSE) katika mazingira ya karakana au mgodini.
- Awe tayari kujifunza zaidi na kuboresha ujuzi wake kwa mafunzo ya daraja la juu (Daraja II na I).
- Leseni ya udereva daraja C au E kutoka katika chuo kinachotambulika.
- Awe na umri usiozodi miaka 30.

**NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**

- Maombi yaelekezwe kwa:
  **Afisa Rasilimali Watu**
  Matundasi ASM Development Company Limited,
  S.L.P 70812,
  DAR ES SALAAM,
- Maombi yote yatumwe kupitia barua pepe info@matundasiasm.co.tz na hr@matundasiasm.co.tz
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20 Juni, 2025,** na kichwa cha barua pepe kiwe jina la nafasi unayoomba.

**VIAMBATANISHO MUHIMU**

- Waombaji wenye sifa wanatakiwa kuwasilisha barua ya maombi ikiwa na nyaraka zifuatazo:
    a) Nakala za vyeti husika (vilivyothibitishwa),
    b) Nakala ya leseni
    c) Nakala ya cheti Cha utumishi (kampuni aliyotoka)
    d) Picha mbili (2) za pasipoti za hivi karibuni,
    e) Wasifu binafsi (CV)
    f) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA)
    g) Police Fingerprint.
    h) Wadhamini watatu (wa nje na ndani ya familia ikiwa na picha za wadhamini na anuani zao (nambari za simu)
    i) Barua ya wadhamini watatu, mmoja (01) wa nje na wawili (02) wa familia pamoja na picha(passport) zao na mawasiliano yao yanayopatikana.
    j) Barua ya utambulisho kutoka serikali za mtaa anapotokea.
- Waombaji waliotimiza vigezo ndio watakaoitwa kwa ajili ya usaili.

MATUNDASI
ASM
COMPANY
LTD